*Re-aranged and translated by Pastor Stephen Letta*

**Enock Maguru, (1921–2011)**

Enock Barandaje Maguru alikuwa mwanzilishi wa Uadventista katika mkoa wa Kigoma, Tanzania.

**Maisha ya Awali na Uongofu**

Enock Barandaje Maguru alizaliwa mwaka 1921 katika kijiji cha Munanila mkoani Kigoma nchini Tanzania. Wazazi wake walikuwa ni wenyeji wa mkoa wa Kigoma. Baba yake alikuwa Majoro na mama yake Nyakiki. Walikuwa na watoto 13 ambao ni Sadock, Enikia, Bertha, Underson, Yohosheba, Lotani, Benjamin, Ishmael, Nsekakaliho, Zawadi, Nyamdogwa, Nyabenda, na Buchumi. Enock Maguru alitumia maisha yake ya utotoni katika kijiji cha Munanila mkoani Kigoma. Alisoma Shule ya Msingi Kangara iliyopo Morogoro, lakini hakumaliza darasa la nane. Aliacha shule katika darasa la sita baada ya kuugua kwa muda.

Mchungaji Sparrow, mmishionari kutoka Afrika Kusini, alikuja mkoani Kigoma mwaka 1946. Alifanya urafiki na Enock Maguru ambaye alikuwa miongoni mwa Waafrika saba wa kwanza waliobatizwa huko Kigoma mwaka 1948.

**Ndoa**

Akiwa na umri wa miaka 22, Enock Maguru alioa mke wake wa kwanza, aitwaye Mchulila au Ada. Mke huyo alikufa mnamo mwaka 1955 na kumwacha na watoto watatu. Enock Maguru alioa mke wake mwingine baada ya kufiwa mnamo mwaka 1956 na wakapata watoto kumi.

Maguru alifadhiliwa na Hospitali ya Misheni ya Heri kwa masomo ya juu ya matengenezo ya jumla. Mnamo Desemba 19, 1965, alimaliza kozi hiyo na kutunukiwa cheti kutoka Shule ya Viwanda ya Matandani nchini Malawi.

**Uchungaji**

Enock Maguru alikuwa mzee wa kanisa mahalia, mwinjilisti, na mtegemezi wa kanisa. Alisimamia ujenzi wa makanisa ya mtaa wa Nyamasovu na Karo. Aliendesha mikutano kadhaa ya hadhara ya uinjilisti na kufadhili wahubiri wengine. Alikuwa mwanzilishi wa Uadventista mkoani Kigoma.

Enock Maguru alimsaidia Sparrow katika ujenzi na kushiriki katika ujenzi wa barabara na katika kujenga Hospitali ya Misheni ya Heri. Baada ya Sparrow kuondoka nchini, Enock Maguru alikuwa fundi mkuu wa Hospitali ya Misheni ya Heri.

**Maisha ya Baadaye**

Enock Maguru alistaafu mwaka 1983 kama fundi mkuu wa Hospitali ya Heri Adventist. Alipokea tuzo kadhaa na kutambuliwa kwa mchango wake bora. Divisheni ya Afrika Mashariki ilimtunuku cheti cha kutambua huduma bora na utumishi uliotukuka na usio

na ubinafsi kwa kazi ya afya ya Kanisa Barani Afrika. Pia alipokea tuzo kutoka kwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, rais wa kwanza wa Tanzania. Alitambuliwa Desemba 9, 1968, kwa kuwa mtu wa kwanza mkoani Kigoma kuendeleza kilimo na ufugaji wa kisasa. Enock Maguru alifariki dunia Septemba 11, 2011 huko Karo katika kijiji cha Munanila, wilayani Buhigwe, mkoani Kigoma nchini Tanzania.